**BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR**

# TATHMINI YA UFAULU WA WATAHINIWA WALIOFANYA MTIHANI WA KUINGILIA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2023

**108 KIARABU**

Kimetayarishwa na

Baraza la Mitihani la Zanzibar

S. L. P. 3070,

Zanzibar.

©Baraza la Mitihani la Zanzibar, 2024

Haki zote zimehifadhiwa

# YALIYOMO

DIBAJI ... iv
1.0 UTANGULIZI ... 1
2.0 SAMPULI YA WATAHINIWA ... 1
3.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI ... 1
3.1 SEHEMU A: KUSOMA NA KUFAHAMU ... 1
3.1.1 Swali la 1: Ufahamu ... 1
3.1.2 Swali la 2: Ufahamu ... 5
3.2 SEHEMU B: KANUNI ZA LUGHA NA MATUMIZI ... 7
3.2.1 Swali la 3: Aina za maneno (المذكر والمؤنث) ... 8
3.2.2 Swali la 4: Uundaji ... 10
3.2.3 Swali la 5: Kupanga maneno ... 11
3.2.4 Swali la 6: Sentensi ... 13
3.2.5 Swali la 7: Nambari ... 15
3.3 SEHEMU C: FASIHI (الأدب) ... 17
3.3.1 Swali la 8: Methali na Hekima ... 17
3.3.2 Swali la 9: Vitendawili ... 19
3.4. SEHEMU D: UTUNGAJI (التعبير) ... 21
3.4.1 Swali la 10: Utungaji ... 21
4.0 HITIMISHO ... 24
5.0 MAPENDEKEZO ... 24
VIAMBATANISHO ... 26

# DIBAJI

Baraza la Mitihani la Zanzibar limeandaa taarifa ya ufaulu wa watahiniwa wa Mtihani wa Kuingilia Kidato cha Kwanza katika somo la Kiarabu Mwaka 2023. Taarifa hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho wa ufaulu kwa wanafunzi, walimu, wazazi, waandaaji wa sera, watunga mitaala na jamii kwa ujumla kuhusu ufaulu wa watahiniwa kwa somo hilo.

Mtihani wa Kuingilia Kidatu cha Kwanza ni kigezo cha miaka mitatu ya Elimu ya Msingi ambapo wanafunzi hupimwa ni kwa kiasi gani wameweza kufahamu masomo yao ya Darasa la tano (5) hadi la saba (7). Hivyo, mtihani huu ni maandalizi tosha kwa ajili ya Elimu ya Sekondari ya Awali.

Uchambuzi uliowasilishwa katika ripoti hii, unakusudia kuonesha tathmini juu ya majibu ya Watahiniwa katika somo la Kiarabu. Ripoti inabainisha sababu tofauti zilizosababisha watahiniwa kujibu vizuri au vibaya. Miongoni mwa sababu za watahiniwa kufanya vizuri ni kuwa na ufahamu mzuri kwa mada mbalimbali zilizoulizwa na umahiri katika kusoma na kuandika lugha ya Kiarabu.

Aidha, watahiniwa walijibu vibaya kwa baadhi ya maswali kwa sababu zifuatazo, kutokuwa na uwelewa mzuri wa matakwa ya maswali, kukosa maarifa juu ya mada zilizojitokeza katika mtihani, kutokuwa na msamiati wa kutosha wa lugha ya Kiarabu na hawakuwa na umahiri wa kusoma na kuandika lugha ya Kiarabu.

Kwa kuendelea zaidi, uchambuzi umeonesha vielelezo vya watahiniwa jinsi walivyojibu vizuri au vibaya. Mwisho, uchambuzi huu umetumia jadweli ambazo zimebainishwa kwa rangi tofauti. Jadweli hizo zinaonesha ufaulu wa watahiniwa hao kwa kila swali.

Kwa hiyo, ni imani ya Baraza kuwa mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti hii yatachukuliwa na wadau wa Elimu na kuyafanyia kazi kwa lengo la kuinua ufaulu wa somo la Kiarabu katika Mitihani yote inayoandaliwa na Baraza la Mitihani la Zanzibar.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Zanzibar linatoa shukurani kwa Maafisa wa Mitihani na wote walioshiriki katika kukamilisha Taarifa hii.

**Dkt. RASHID .A. MUKKI**



**MKURUGENZI**
**BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR**
**ZANZIBAR**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa ya uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa wa Mtihani wa kuingilia Kidato cha Kwanza kwa somo la Kiarabu mwaka 2023. Mtihani ulitungwa kwa kuzingatia muhtasari wa Zanzibar wa mwaka 2009 na 2022 na kufuata muundo wa mtihani wa Darasa la Saba wa Baraza la Mitihani la Zanzibar wa mwaka 2022.

Mtihani wa Kiarabu ulikuwa na maswali kumi (10) yaliyogawanyika katika Sehemu A, B, C na D kwa kuzingatia mada ya Ufahamu, Kanuni za Lugha na Matumizi ya Lugha, Utungaji na Fasihi. Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote katika kila sehemu.

## 2.0 SAMPULI YA WATAHINIWA

Idadi ya watahiniwa waliofanyiwa Tathmini ni **4,548** sawa na asilimia **10.42** ya watahiniwa **43,640** waliosajiliwa kufanya mtihani wa somo hili. Uchambuzi kwa kila swali ulizingatia viwango vitatu vya ufaulu ambavyo ni vibaya, wastani na vizuri ambapo vibaya ulianza alama 0 hadi 20, wastani 21 hadi 60 na vizuri 61 hadi 100. Ufaulu huo umeoneshwa kupitia jadweli kwa kutumia rangi tatu ambazo ni: Kijani inawakilisha vizuri, manjano inawakilisha wastani na nyekundu inawakilisha vibaya.

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI

Sehemu hii, inaonesha maswali yaliyojibiwa na watahiniwa katika sehemu A, B, C na D. Pia inawakilisha idadi na asilimia ya watahiniwa waliojibu maswali pamoja na waliopata vibaya, wastani na vizuri. Mwisho, vielelezo vya watahiniwa waliojibu vizuri na vibaya vimeambatanishwa

### 3.1 SEHEMU A: KUSOMA NA KUFAHAMU

Sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama ishirini (20) zilizogawanywa katika maswali mawili ambapo kila swali lilikuwa na alama 10.Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu hii.

#### 3.1.1 Swali la 1: Ufahamu

Swali la kwanza lilitokana na mada ya ufahamu ambapo mtahiniwa alitakiwa kusoma habari aliyopewa kisha kujibu maswali yaliyotokana na habari hiyo. Swali hili lilikuwa na vipengele vitano (5) kuanzia (أ) hadi (هـ).

Kipengele (أ) cha swali kilimtaka mtahiniwa kueleza nini anafanya unapokaribia mwaka mpya.

Kipengele (ب) kilimtaka mtahiniwa kueleza ama kutaja alichosema mwalimu mkuu alipokuja skuli kwa ugawaji wa vyeti na zawadi.

Kipengele (ج) kilimtaka mtahiniwa kueleza vipi walienda wanafunzi katika skuli zao.

Kipengele (د) kilimtaka mtahiniwa kueleza na kutoa sababu kwa nini wanafunzi walipongezana wao kwa wao.

Kipengele (ه) kilimtaka mtahiniwa kueleza na kuandika walichofanya wanafunzi baada ya kusoma dua ya asubuhi.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima ufahamu na maarifa ya mtahiniwa katika kusoma habari na kujibu maswali kulingana na habari husika.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **4,362** sawa na asilimia **95.91**, na watahiniwa **186** sawa na asilimia **4.09** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 1a.

**Jadweli nambari 1a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA 0 – 2 | | WASTANI 2.5 - 6 | | VIZURI 6.5 – 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,298 | 29.76 | 1,417 | 32.49 | 1647 | 37.75 | 3,064 | 70.24 |

Takwimu za jadweli nambari 1a zinaonesha kuwa asilimia ya kati ya ufaulu wa **37.75** upo katika kiwango kizuri ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa mzuri kwa asilimia **70.24.**

Aidha, watahiniwa **1,298** sawa na asilimia **29.76** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 1.1.

**Kielelezo1.1 (Kibaya)`**

أ- مَاذَا تَفْعَلُ إِذَا اِقْتَرَبَ الْعَامُ الدِّرَاسِيُّ الْجَدِيْدُ؟

وَيَقْرَ قِرَاءَةِ الدُّعَاءِ

ب- مَاذَا قَالَ الْمُدِيْرُ حِيْنَمَا جَاءَ فِيْ الْمَدْرَسَةِ لِيُوَزِّعَ عَلَى التَّلَامِيْذِ الشَّهَادَاتِ وَجَوَائِزَ التَّفَوُّقِ؟

وَأَقْلَامِ وَغَيْرِهَا مِمَّا تَحْتَاجُ فِي دِرَاسَتِهِ

ج- كَيْفَ ذَهَبَ التَّلَامِيْذُ إِلَى مَدَارِسِهِمْ؟

وَغَدًا أَنْقُو إِلَى الْمَدْرَسَةِ مِنْ جَدِيْدٍ.

د- لِمَاذَا هَنَّأَ التَّلَامِيْذُ بَعْضُهُمْ بَعْضًا؟

فَبَدَأَ الْعَامُ الدِّرَاسِيُّ الْجَدِيْدُ بِقُوَّةٍ وَنَشَاطٍ

هـ- مَاذَا فَعَلَ التَّلَامِيْذُ بَعْدَ قِرَاءَةِ الدُّعَاءِ الصَّبَاحِيِّ؟

وَأَوْ كُلٌّ وَاحِدٍ يُهَنِّئُ الزُّمَلَاءَ

Kielelezo 1.1 ni mfano wa mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa hakufahamu habari aliyosoma, hivyo hakuweza kujibu vizuri maswali aliyotakiwa kujibu, bali hata alichokiandika hakifahamiki.

**Kielelezo 1.2 (Kizuri)**

أ- مَاذَا تَفْعَلُ إِذَا اِقْتَرَبَ الْعَامُ الدِّرَاسِيُّ الْجَدِيْدُ؟

إِذَا اِقْتَرَبَ الْعَامُ الدِّرَاسِيُّ الْجَدِيْدُ كُلُّ تِلْمِيْذٍ يَشْتَرِي مَا يَلْزِمُهُ مِنَ الْعَامِ الْجَدِيْدِ

ب- مَاذَا قَالَ الْمُدِيْرُ حِيْنَمَا جَاءَ فِيْ الْمَدْرَسَةِ لِيُوَزِّعَ عَلَى التَّلَامِيْذِ الشَّهَادَاتِ وَجَوَائِزَ التَّفَوُّقِ؟

قَالَ الْمُدِيْرُ حِيْنَمَا جَاءَ فِي الْمَدْرَسَةِ "يَا اَبْنَائِي، أَتَمَنَّى لَكُمْ عُطْلَةً سَعِيْدَةً"

ج- كَيْفَ ذَهَبَ التَّلَامِيْذُ إِلَى مَدَارِسِهِمْ؟

ذَهَبَ التَّلَامِيْذُ إِلَى مَدَارِسِهِمْ نَشِيْطِيْنَ مَسْرُوْرِيْنَ

د- لِمَاذَا هَنَّأَ التَّلَامِيْذُ بَعْضُهُمْ بَعْضًا؟

هَنَّأَ التَّلَامِيْذُ بَعْضُهُمْ بَعْضًا بِسَلَامَةِ الْعَوْدَةِ إِلَى الْمَدْرَسَةِ

هـ- مَاذَا فَعَلَ التَّلَامِيْذُ بَعْدَ قِرَاءَةِ الدُّعَاءِ الصَّبَاحِيِّ؟

فَعَلَ التَّلَامِيْذُ بَعْدَ قِرَاءَةِ الدُّعَاءِ الصَّبَاحِيِّ دَخَلُوْا الْفُصُوْلَ

Kielelezo 1.2 ni mfano wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali husika. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa alifahamu vizuri habari aliyosoma, hivyo aliweza kujibu vizuri maswali aliyotakiwa kujibu.

**3.1.2 Swali la 2: Ufahamu**

Swali la pili lilitokana na mada ya ufahamu ambapo mtahiniwa pia alitakiwa kusoma habari aliyopewa kisha kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuchagua jibu sahihi miongoni mwa jawabu alizopewa. Swali hili lilikuwa na vipengele vitano (5) kuanzia (أ) hadi (ه).

Kipengele cha kwanza hadi cha tano vilimtaka mtahiniwa kujaza neno lililokosekana katika ibara husika kwa kuchagua jibu au neno sahihi miongoni mwa majibu au maneno aliyopewa.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima ufahamu na maarifa ya mtahiniwa katika kusoma habari na kujibu maswali kulingana na habari husika Pamoja na umakini wa kuchagua jibu sahihi miongoni mwa majibu aliopewa.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **4,488** sawa na asilimia **98.68** na watahiniwa **60** sawa na asilimia **1.32** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 1b.

**Jadweli nambari 1b: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA 0 – 2 | | WASTANI 2.5 - 6 | | VIZURI 6.5 – 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,484 | 33.07 | 1,191 | 26.53 | 1,813 | 40.40 | 3,004 | 66.93 |

Takwimu za jadweli nambari 1b zinaonesha kuwa asilimia ndogo ya ufaulu wa **33.07** upo katika kiwango cha chini ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa mzuri kwa asilimia **66.93.**

Aidha, watahiniwa **1,484** sawa na asilimia **33.07** wamepata ufaulu mbaya.Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 2.1

**Kielelezo 2.1 (Kibaya)**

٢. اِمْلَأِ الْفَرَاغَاتِ بِوَضْعِ إِجَابَةٍ صَحِيْحَةٍ مِمَّا بَيْنَ الْقَوْسَيْنِ كَمَا وَرَدَ فِيْ الْقِصَةِ السَّابِقَةِ.

أ- بَدَأَ التَّلَامِيْذُ يَجْلِسُوْنَ للدِّرَاسَةِ.

(يَذْهَبُوْنَ - يَسْتَعِدُّوْنَ - يُجَهِّزُوْنَ - يَجْلِسُوْنَ).

ب- ذَهَبَ التَّلَامِيْذُ إِلَى مَنَازِلِهِمْ.

(مَنَازِلِهِمْ - زُمَلَائِهِمْ - مَدَارِسِهِمْ - بَسَاتِيْنِهِمْ)

ج- وَقَفَ التَّلَامِيْذُ لِتلميذ الصَّبَاحِيِّ.

(الدُّعَاءِ - الطَّابُوْرِ - الْعَمَلِ - الدَّرْسِ).

د- اِشْتَرَى كُلُّ تِلْمِيْذٍ دَفَاتِرَ وَكُتُبًا


(دَفَاتِرَ وَكُتُبًا - أَقْلَامًا وَكُتُبًا - مَا يَلْزَمُهُ - زَيًّا مَدْرَسِيًّا).

هـ- يَا أَبْنَائِيْ أَتَمَنَّى لَكُمْ سُرْعَةً شَدِيْدَةً.

(سَلَامَةَ الْعَوْدَةِ - صِحَةً طَيِّبَةً - عُطْلَةً سَعِيْدَةً - سُرْعَةً شَدِيْدَةً).

Kielelezo 2.1 ni mfano wa mtahiniwa aliyeshindwa kujibu vizuri swali husika. Mtahiniwa huyu anaonekana kuwa hakufahamu habari aliyosoma, hivyo hakuweza kujibu vizuri maswali aliyotakiwa kujibu kwa kuchagua jibu sahihi.

**Kielelezo 2.2 (Kizuri)**



٢. اِمْلَأِ الْفَرَاغَاتِ بِوَضْعِ إِجَابَةٍ صَحِيْحَةٍ مِمَّا بَيْنَ الْقَوْسَيْنِ كَمَا وَرَدَ فِيْ الْقِصَّةِ السَّابِقَةِ.

أ- بَدَأَ التَّلَامِيْذُ يَسْتَعِدُّوْنَ لِلدِّرَاسَةِ.

(يَذْهَبُوْنَ - يَسْتَعِدُّوْنَ - يُجَهِّزُوْنَ - يَجْلِسُوْنَ).

ب- ذَهَبَ التَّلَامِيْذُ إِلَى مَدَارِسِهِمْ.

(مَنَازِلِهِمْ - زُمَلَائِهِمْ - مَدَارِسِهِمْ - بَسَاتِيْنِهِمْ)

ج- وَقَفَ التَّلَامِيْذُ لِـ الدُّعَاءِ الصَّبَاحِيِّ.

(الدُّعَاءِ - الطَّابُوْرِ - الْعَمَلِ - الدَّرْسِ).

د- اِشْتَرَى كُلُّ تِلْمِيْذٍ مَا يَلْزَمُهُ.

(دَفَاتِرَ وَكُتُبًا - أَقْلَامًا وَكُتُبًا - مَا يَلْزَمُهُ - زَيًّا مَدْرَسِيًّا).

هـ- يَا أَبْنَائِيْ أَتَمَنَّى لَكُمْ عُطْلَةً سَعِيْدَةً.

(سَلَامَةَ الْعَوْدَةِ - صِحَّةً طَيِّبَةً - عُطْلَةً سَعِيْدَةً - سُرْعَةً شَدِيْدَةً).

Kielelezo nambari 2.2 kinaonesha namna mtahiniwa alivyojibu vizuri swali hili na kuonekana kuwa anauelewa mzuri wa kusoma na kufahamu habari aliyotakiwa kuisoma, bali pia anaonekana kuwa na umakini wa kuchagua majibu sahihi kulingana na kifungu cha habari alichopewa. Mtahiniwa huyu ameweza kuchagua majibu sahihi yaliyotakiwa katika kila kipengele cha swali husika. Hivyo, majibu yake yalikidhi mahitaji ya swali hilo.

## 3.2 SEHEMU B: KANUNI ZA LUGHA NA MATUMIZI

Sehemu hii ilikuwa na maswali matano (5): Swali la tatu (3) hadi la saba (7) kutoka katika mada ya Kanuni za Kilugha. Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote matano na kila swali lilikuwa na alama kumi (10), hivyo ni jumla ya alama hamsini zinapatikana katika sehemu hii. Uchambuzi kwa kila swali katika sehemu hii umezingatia viwango vitatu (3) vya ufaulu, ambavyo ni vizuri, wastani na vibaya. Ufaulu mzuri umeanza

alama 6.5 hadi alama 10, ufaulu wa wastani ulilikuwa ni alama 2.5 mpaka alama 6 na ufaulu mbaya (kiwango cha chini) ulianza alama 0 hadi alama 2.

**3.2.1 Swali la 3: Aina zamaneno (المذكر والمؤنث)**

Swali la tatu lilitokana na mada ya aina za maneno ambapo mtahiniwa alitakiwa kuainisha maneno yaliyopigiwa mistari. Swali hili lilikuwa na vipengele vitano (5) kuanzia (أ) hadi (هـ).

Kipengele cha kwanza hadi cha tano vilimtaka mtahiniwa kuainisha maneno yaliyopigiwa mstari chini katika ibara husika kwa kuyaweka maneno ya **مؤنث** katika orodha yake.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika utumiaji mzuri wa maneno.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **4,209** sawa na asilimia **92.55** na watahiniwa **339** sawa na asilimia **7.45** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 2a.


**Jadweli nambari 2a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA 0 – 2 | | WASTANI 2.5 - 6 | | VIZURI 6.5 – 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,017 | 24.16 | 1,804 | 42.86 | 1,388 | 32.98 | 3,192 | 75.84 |

Takwimu za Jadweli nambari 2a zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **42.86** upo katika kiwango cha wastani ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa mzuri kwa asilimia **75.84.**


Aidha, watahiniwa **1,017** sawa na asilimia **24.16** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 3.1.

**Kielelezo 3.1 ( Kibaya)**




Kielelezo nambari 3.1 kinaonesha mfano wa mtahiniwa aliyeshindwa kutoa majibu sahihi kwa kutokidhi matakwa ya swali kwani mtahiniwa alishindwa kuweka na kupanga kwa usahihi majina aliyopewa katika kila kipengele cha swali hili na kuyaweka katika orodha husika kama alivyotakiwa kufanya.

**Kielelezo 3.2 ( Kizuri)**



| المؤنث | المذكر | |
|---|---|---|
| السماوات | الطفل | أ- |
| رجلين | ديك | ب- |
| الأم | محمد | ج- |
| القافلة | | د- |
| أخوات | | هـ- |
| الصحراء | | و- |

Kielelezo nambari 3.2 kinaonesha mfano wa mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi na kukamilisha matakwa ya swali kwani aliweza kuweka na kupangiliya majina aliyopewa katika kila kipengele cha swali hili na kuyaweka katika orodha husika kama alivyotakiwa kufanya. Hali hii inaonesha kuwa mtahiniwa anauelewa mzuri juu ya mada ya mudhakari na muannathi "المذكر والمؤنث".

### 3.2.2 Swali la 4: Uundaji

Swali la nne lilitokana na mada ya uundaji ambapo mtahiniwa alitakiwa kuunda sentensi kwa mujibu wa maelekezo aliyopewa. Swali hili lilikuwa na vipengele vitano (5) kuanzia (أ) hadi (هـ).

Kipengele cha kwanza hadi cha tano, vilimtaka mtahiniwa kusahihisha maneno yaliyopigiwa mstari chini katika ibara husika.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika uundaji sahihi wa sentensi kwa kuzingatia matumizi sahihi ya maneno.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **4,154** sawa na asilimia **91.34** na watahiniwa **394** sawa na asilimia **8.66** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 2b.


**Jadweli nambari 2b: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA 0 – 2 | | WASTANI 2.5 - 6 | | VIZURI 6.5 – 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 3,800 | 91.48 | 286 | 6.88 | 68 | 1.64 | 354 | 8.52 |

Takwimu za Jadweli nambari 2b zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **91.48** upo katika kiwango cha chini ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa mbaya kwa asilimia **8.52.**

Aidha, watahiniwa **3,800** sawa na asilimia **91.48** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 4.1

**Kielelezo 4.1 ( Kibaya)**



٤. صَحِّحِ الْكَلِمَاتِ الَّتِي تَحْتَهَا خَطٌّ مِنَ الْجُمَلِ الْآتِيَةِ:

أ - هَذِهِ تِلْمِيْذًا تَجْتَهِدُ فِيْ دُرُوْسِهَا. ______

ب - أَنْتُمْ تَذْهَبْنَ إِلَى الْمَدْرَسَةِ. ______


ج - أَنْتِ تَجْلِسُ عَلَى كُرْسِيِّكِ. ______

د - هَذَا شَجَرَتَانِ مُثْمِرَتَانِ. ______

هـ - اَلْحُجَّاجُ يَذْهَبُ إِلَى بَيْتِ الْعَتِيْقِ. ______

Kielelezo nambari 4.1 kinaonesha mfano wa mtahiniwa aliyeshindwa kutoa majibu sahihi kwa kutokidhi matakwa ya swali kwani mtahiniwa alishindwa kusahihisha sentensi alizotakiwa kufanya hivyo katika kila kipengele cha swali hili.

**Kielelezo 4.2 ( Kizuri)**



٤. صَحِّحِ الْكَلِمَاتِ الَّتِي تَحْتَهَا خَطٌّ مِنَ الْجُمَلِ الْآتِيَةِ:

أ - هَذِهِ تِلْمِيْذًا تَجْتَهِدُ فِيْ دُرُوْسِهَا. تِلْمِيْذَةٌ

ب - أَنْتُمْ تَذْهَبْنَ إِلَى الْمَدْرَسَةِ. تَذْهَبُوْنَ

ج - أَنْتِ تَجْلِسُ عَلَى كُرْسِيِّكِ. تَجْلِسِيْنَ

د - هَذَا شَجَرَتَانِ مُثْمِرَتَانِ. هَاتَانِ

هـ - اَلْحُجَّاجُ يَذْهَبُ إِلَى بَيْتِ الْعَتِيْقِ. يَذْهَبُوْنَ

Kielelezo nambari 4.2 kinaonesha mfano wa mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi na kukamilisha matakwa ya swali kwani aliweza kusahihisha sentensi hizo kwa usahihi katika kila kipengele cha swali hili. Hali hii inaonesha kuwa mtahiniwa anauelewa mzuri juu ya mada husika.

### 3.2.3 Swali la 5: Kupanga maneno

Swali la tano lilitokana na mada ya uundaji wa sentensi ambapo mtahiniwa alitakiwa kuunda sentensi kwa mujibu wa maelekezo aliyopewa. Swali hili lilikuwa na vipengele vitano (5) kuanzia (أ) hadi (هـ).

Kipengele cha kwanza hadi cha tano, vilimtaka mtahiniwa kupanga maneno yaliyoparaganywa ili kuunda sentensi sahihi zenye maana kamili.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika uundaji sahihi wa sentensi kwa kuzingatia matumizi sahihi ya maneno.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **4,230** sawa na asilimia **93.01** na watahiniwa **318** sawa na asilimia **6.99** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 2c.


**Jadweli nambari 2c: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 – 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 2,171 | 51.32 | 1,560 | 36.88 | 499 | 11.80 | 2,059 | 48.68 |

Takwimu za jadweli nambari 2c zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **51. 32** upo katika kiwango cha chini ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa wa wastani kwa asilimia **48.68.**

Aidha, watahiniwa **2,171** sawa na asilimia **51.32** wamepata ufaulu mbaya.watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 5.1

**Kielelezo 5.1 ( Kibaya)**


٥. رَتِّبِ الْكَلِمَاتِ الْآتِيَةَ لِتُصْبِحَ جُمَلاً مُفِيْدَةً.

أ ـ إِلَى ـ سَوْفَ ـ السَّلاَمِ ـ أُسَافِرُ ـ دَارِ.

أُسَافِرُ دَارِ سَوْفَ إِلَى السَّلاَمِ.

ب ـ يَا ـ النُّوْرِ ـ مَسَاءُ ـ وَالِدِيْ؟

وَالِدِيْ النُّوْرِ مَسَاءُ يَا.

ج ـ إِسْمُ ـ مَا ـ مَدْرَسَتُكَ؟

مَدْرَسَتُكَ مَا إِسْمُ.

د ـ اللُّغَةَ ـ أَنَا ـ الْعَرَبِيَّةَ ـ أَتَعَلَّمُ.


أَنَا الْعَرَبِيَّةَ اللُّغَةَ.

هـ ـ بَيْتُ ـ صَالِحٍ ـ هَذَا ـ لِشَيْخٍ.

لِشَيْخٍ هَذَا صَالِحٍ بَيْتُ.

Kielelezo nambari 5.1 kinaonesha mfano wa mtahiniwa aliyeshindwa kutoa majibu sahihi kwa kutokidhi matakwa ya swali. Mtahiniwa alishindwa kupanga maneno na kuunda sentensi sahihi zenye maana kama alivyotakiwa kufanya katika kila kipengele cha swali husika.

**Kielelezo 5.2 ( Kizuri)**


٥. رَتِّبِ الْكَلِمَاتِ الْآتِيَةَ لِتُصْبِحَ جُمَلاً مُفِيْدَةً.

أ - إِلَى - سَوْفَ - السَّلَامِ - أُسَافِرُ - دَارِ.

سَوْفَ أُسَافِرُ إِلَى دَارِ السَّلَامِ.

ب - يَا - النُّوْرِ - مَسَاءُ - وَالِدِيْ؟

مَسَاءُ النُّوْرِ يَا وَالِدِيْ؟

ج - اِسْمُ - مَا - مَدْرَسَتِكَ؟

مَا اِسْمُ مَدْرَسَتِكَ؟

د - اللُّغَةَ - أَنَا - الْعَرَبِيَّةَ - أَتَعَلَّمُ.

أَنَا أَتَعَلَّمُ اللُّغَةَ الْعَرَبِيَّةَ.

هـ - بَيْتُ - صَالِحٍ - هَذَا - لِشَيْخٍ.

هَذَا بَيْتُ لِشَيْخٍ صَالِحٍ.

Kielelezo nambari 5.2 kinaonesha mfano wa mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi na kukamilisha matakwa ya swali kwani aliweza kupanga sentensi hizo kwa usahihi na kuleta maana sahihi katika kila kipengele cha swali hili. Hali hii inaonesha kuwa mtahiniwa anauelewa mzuri juu ya mada ya uundaji.

**3.2.4 Swali la 6: Sentensi**

Swali la sita lilitokana na mada ya uchambuzi wa sentensi ambapo mtahiniwa alitakiwa kuirabu maneno yaliyopigiwa msatri katika sentensi. Swali hili lilikuwa na vipengele vitano (5) kuanzia (أ) hadi (هـ).

Kipengele cha kwanza hadi cha tano, vipengele hivyi vilimtaka mtahiniwa kuirabu au kuchambua aina za maneno yaliyopigiwa mstari chini katika sentensi alizotakiwa kufanya hivyo.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika uchambuzi sahihi wa sentensi kwa kuzingatia maagizo aliyopewa.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **3,889** sawa na asilimia **85.51**, na watahiniwa **659** sawa na asilimia **14.49** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 2d.


**Jadweli nambari 2d: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA 0 – 2 | | WASTANI 2.5 - 6 | | VIZURI 6.5 – 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 2,762 | 71.02 | 560 | 14.40 | 567 | 14.58 | 1,127 | 28.98 |

Takwimu za jadweli nambari 2d zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **71.02** upo katika kiwango kibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa wastani kwa asilimia **28.98.**

Aidha, watahiniwa **2,762** sawa na asilimia **71.02** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 6.1

**Kielelezo 6.1 ( Kibaya)**




Kielelezo nambari 6.1 kinaonesha mfano wa mtahiniwa aliyeshindwa kuchambua sentensi alizopewa kwa usahihi kwani hakuweza kuirabu aina za maneno alizotakiwa kuziirabu katika sentensi alizopewa katika kila kipengele cha swali husika.

**Kielelezo 6.2 ( Kizuri)**

٦. أعْرِبْ مَا تَحْتَهُ خَطٌّ:

أ - اَلنَّظَافَةُ وَاجِبَةٌ.

النَّظَافَةُ: مبتدأ مرفوع وعلامة رفعه ضمة ظاهرة على آخره.

ب - لَا تَلْعَبْ بِالنَّارِ.

النَّارِ: إسم مجرور ببا وعلامة جره كسرة ظاهرة على آخره.

ج - دَقَّتِ الْبِنْتُ الْجَرَسَ.

الْجَرَسَ: مفعول به منصوب وعلامة نصبه فتحة ظاهرة على آخره.

د - وَقَفَ الرَّجُلُ أَمَامَ بَيْتِنَا.

وَقَفَ: فعل الماضي مبني على الفتح.

هـ - سَافَرَ عَلِيٌّ إِلَى مُمْبَا.

عَلِيٌّ: فاعل مرفوع وعلامة رفعه ضمة ظاهرة على آخره.

Kielelezo nambari 6.2 kinaonesha mfano wa mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi na kukamilisha matakwa ya swali kwani aliweza kuirabu aina za maneno kwa usahihi kama alivyotakiwa kufanya. Hali hii inaonesha kuwa mtahiniwa alikuwa na uwelewa mzuri juu ya mada ya uchambuzi.

### 3.2.5 Swali la 7: Nambari

Swali la saba lilitokana na mada ya nambari ambapo mtahiniwa alitakiwa kuandika nambari kwa usahihi. Swali hili lilikuwa na vipengele vitano (5) kuanzia (أ) hadi (هـ).

Kipengele cha kwanza hadi cha tano, vilimtaka mtahiniwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuandika nambari kimaneno au kitarakimu, kulingana na maelekezo aliyopewa.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika uandishi na usomaji sahihi wa nambari alizopewa.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **4,083** sawa na asilimia **89.78**, na watahiniwa **465** sawa na asilimia **10.22** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 2e.


**Jadweli nambari 2e: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 – 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 2,965 | 72.62 | 825 | 20.20 | 293 | 7.18 | 1,118 | 27.38 |

Takwimu za jadweli nambari 2e zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **72.62** upo katika kiwango kibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa wastani kwa asilimia **27.38.**


Aidha, watahiniwa **2,762** sawa na asilimia **71.02** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 7.1.

**Kielelezo 7.1 ( Kibaya)**




Kielelezo nambari 7.1 kinaonesha mfano wa mtahiniwa aliyeshindwa kuandika kwa ushihi nambari alizotakiwa kuziandika kimaandishi ama kitarakimu kwa mujibu wa maelezo aliyopewa katika kila kipengele cha swali husika.

**Kielelezo 7.2 ( Kizuri)**


٧. إِمْلَإِ الْفَرَاغَاتِ الْآتِيَةَ بِأَرْقَامٍ أَوْ كَلِمَاتٍ مُنَاسِبَةٍ.

أ - ٦٣٥ خَمْسٌ وَثَلَاثُونَ وَسِتَّةُ مِائَةٍ.

ب - ٧٠١ وَاحِدٌ وَسَبْعُ مِائَةٍ.

ج - ٨٥٤ أَرْبَعٌ وَخَمْسُونَ وَثَمَانُ مِائَةٍ.

د - ٩٠٠ تِسْعَةُ مِائَةٍ.

هـ - ٩٨٠ ثَمَانُونَ وَتِسْعَةُ مِائَةٍ.

Kielelezo nambari 7.2 kinaonesha mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri kwa kuandika majibu hayo vizuri, kwani aliandika nambari alizotakiwa kuziandika kimaandishi ama kitarakimu kwa mujibu wa maelezo aliyopewa katika kila kipengele cha swali husika kwa ushihi. Hali hii inaonesha kuwa mtahiniwa anauelewa mzuri juu ya mada husika.

### 3.3 SEHEMU C: FASIHI (الأدب)

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili (2): Swali la nane (8) na tisa (9) kutoka katika mada ya Fasihi. Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote mawili yaliyokuwa katika sehemu hii. Kila swali lilibeba alama kumi (10), hivyo inafanya jumla ya alama ishirini (20). Viwango vya ufaulu vilivyotumika katika uchambuzi wa sehemu hii ni vitatu (3), yaani vizuri alama 6.5 hadi alama 10, wastani alama 2.5 hadi alama 6 na vibaya alama 0 hadi alama 2.

#### 3.3.1 Swali la 8: Methali na Hekima

Swali la nane lilitokana na mada ya fasihi ambapo mtahiniwa alitakiwa kutoa maana ya methali na hekima alizotakiwa kufanya. Swali hili lilikuwa na vipengele vitano (5) kuanzia (أ) hadi (هـ).

Kipengele cha kwanza hadi cha tano, vilimtaka mtahiniwa kuleta maana ya methali na hekima alizopewa katika kila kipengele cha swali hili.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa na maarifa yake katika utambuzi wa fasihi.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **2,688** sawa na asilimia **59.10**, na watahiniwa **1,860** sawa na asilimia **40.90** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 3a.


**Jadweli nambari 3a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 – 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 2,611 | 97.14 | 67 | 2.49 | 10 | 0.37 | 77 | 2.86 |

Takwimu za jadweli nambari 3a zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **97.14** upo katika kiwango kibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa mbaya kwa asilimia **2.86.**


Aidha, watahiniwa **2,611** sawa na asilimia **97.14** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 8.1.

**Kielelezo 8.1 ( Kibaya)**




Kielelezo nambari 8.1 kinaonesha mfano wa karatasi ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutoa au kuleta maana sahihi za methali na hekima alizotakiwa kutoa katika kila kipengele cha swali husika.

**Kielelezo 8.2 ( Kizuri)**




Kielelezo nambari 8.2 kinaonesha mfano wa mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi na kukamilisha matakwa ya swali kwani aliweza kutoa maana za methali na hekima kwa usahihi kama alivyotakiwa kufanya. Hali hii inaonesha kuwa mtahiniwa alikuwa na uwelewa mzuri juu ya mada ya fasihi.

### 3.3.2 Swali la 9: Vitendawili

Swali la nane lilitokana na mada ya fasihi ambapo mtahiniwa alitakiwa kutegua vitendawili alivyopewa. Swali hili lilikuwa na vipengele vitano (5) kuanzia (أ) hadi (ه).

Kipengele cha kwanza hadi cha tano, vilimtaka mtahiniwa kutegua vitendawili alivyopewa katika kila kipengele cha swali hili.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa na maarifa yake katika utambuzi wa fasihi.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **4,106** sawa na asilimia **90.28** na watahiniwa **442** sawa na asilimia **9.72** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 3b.


**Jadweli nambari 3b: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 – 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 2,950 | 71.84 | 928 | 22.60 | 228 | 5.56 | 1,156 | 28.16 |

Takwimu za Jadweli nambari 3b zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **71.84** upo katika kiwango kibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa wa wastani kwa asilimia **28.16.**

Aidha, watahiniwa **2,950** sawa na asilimia **71.84** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 9.1

**Kielelezo 9.1 ( Kibaya)**


٩. اِخْتَرْ إِجَابَةً صَحِيْحَةً مِنَ اَلْكَلِمَاتِ اَلْآتِيَةِ ثُمَّ اكْتُبْهُ بَيْنَ اَلْقَوْسَيْنِ.

(اَلْبَحْرُ- اَلنَّخِيْلُ – اَلْعُمْرُ – اَلنَّحْلَةُ – اَلسَّفِيْنَةُ – اَلْخَرِيْطَةُ)

أ - جِسْمُهَا صَغِيْرَةٌ تَصْنَعُ اَلْعَسَلَ.

( اَلْعُمْرُ )

ب - تُوْجَدُ بِلَادٌ بِلاَ بَشَرٍ وَبِحَارٌ بِلاَ مَاءٍ وَأَرْضٌ بِلاَ تُرَابٍ.

( اَلْبَحْرُ )

ج - مَا اَلشَّيْءُ اَلَّذِيْ كُلَّمَا زَادَ نَقَصَ؟

( اَلسَّفِيْنَةُ )

د - تَحْمِلُ اَلرُّكَّابَ وَتَجْرِيْ فِيْ اَلْمَاءِ.


( اَلنَّحْلَةُ )

هـ - شَيْءٌ يَسْتَطِيْعُ حَمْلَ قِنْطَارٍ وَلَا يَسْتَطِيْعُ حَمْلَ مِسْمَارٍ.

( اَلْخَرِيْطَةُ )

Kielelezo nambari 9.1 kinaonesha mfano wa karatasi ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutoa majibu sahihi au kutegua kwa usahihi vitendawili alivyopewa katika kila kipengele cha swali husika.

**Kielelezo 9.2 ( Kizuri)**


٩. اِخْتَرْ إِجَابَةً صَحِيْحَةً مِنَ اَلْكَلِمَاتِ اَلْآتِيَةِ ثُمَّ اكْتُبْهُ بَيْنَ اَلْقَوْسَيْنِ.

(اَلْبَحْرُ- اَلنَّخِيْلُ – اَلْعُمْرُ – اَلنَّحْلَةُ – اَلسَّفِيْنَةُ – اَلْخَرِيْطَةُ)

أ - جِسْمُهَا صَغِيْرَةٌ تَصْنَعُ اَلْعَسَلَ.

(النَّحْلَةُ)

ب - تُوْجَدُ بِلَادٌ بِلاَ بَشَرٍ وَبِحَارٌ بِلاَ مَاءٍ وَأَرْضٌ بِلَا تُرَابٍ.

(الْخَرِيْطَةُ)

ج - ما اَلشَّيْءُ اَلَّذِي كُلَّمَا زَادَ نَقَصَ؟

(الْعُمْرُ)

د - تَحْمِلُ اَلرُّكَّابُ وَتَجْرِي فِيْ اَلْمَاءِ.

(السَّفِيْنَة)

هـ - شَيْءٌ يَسْتَطِيْعُ حَمْلَ قِنْطَارٍ وَلَا يَسْتَطِيْعُ حَمْلَ مِسْمَارٍ.

(البَحْرُ)

Kielelezo nambari 9.2 kinaonesha mfano wa karatasi ya majibu ya mtahiniwa aliyewaza kutoa majibu sahihi au kutegua kwa usahihi vitendawili alivyopewa katika kila kipengele cha swali husika.

**3.4. SEHEMU D: UTUNGAJI (التعبير)**

Sehemu hiiilikuwa na swali moja tu, la kumi (10) ambalo lilikuwa na alama 10.

**3.4.1 Swali la 10: Utungaji**

Swali la kumi lilitokana na mada ya utungaji insha au makala ambapo mtahiniwa alitakiwa kupanga sentensi ama ibara alizopewa ili kuunda kisa. Swali hili lilikuwa na vipengele vitano (5) kuanzia (أ) hadi (ه).

Kipengele cha kwanza hadi cha tano, vipengele hivyo vilimtaka mtahiniwa kupanga ibara zilizoparaganywa ili kuunda kisa sahihi chenye maana na mtiririko unaokubalika katika utaratibu wa uandishi wa kisa ama makala.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa utungaji sahihi wa kisa kwa kuzingatia mtiririko maalumu unaokubalika.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **3,182** sawa na asilimia **69.96**, na watahiniwa **1,366** sawa na asilimia **30.04** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli nambari 4a


**Jadweli nambari 4a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA 0 – 2 | | WASTANI 2.5 - 6 | | VIZURI 6.5 – 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,952 | 61.35 | 579 | 18.20 | 651 | 20.45 | 1,230 | 38.65 |

Takwimu za jadweli nambari 4a zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **61.35** upo katika kiwango cha chini ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa wa wastani kwa asilimia **38.65.**

Aidha, watahiniwa **1,952** sawa na asilimia **61.35** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 10.1

**Kielelezo 10.1 ( Kibaya)**




Kielelezo nambari 10.1 kinaonesha mfano wa mtahiniwa aliyeshindwa kutoa majibu sahihi kwa kutokidhi matakwa ya swali. Mtahiniwa alishindwa kupanga sentensi au ibara alizopewa na kuunda kisa sahihi chenye maana na mtiririko unakubalika katika uandishi wa kisa. Hali hii inaonesha kuwa mtahiniwa hakuwa na uelewa mzuri juu ya mada ya uandishi wa Insha.

**Kielelezo 10.2 ( Kizuri)**

١٠. رَتِّبِ ٱلْجُمَلَ ٱلْآتِيَةَ لِتُكَوِّنَ مِنْهَا ٱلْقِصَّةَ.

أ - وَأُنَظِّفُ أَسْنَانِي مَعَ غُسْلِ جِسْمِي.

ب - وَصَلَّيْتُ ٱلصُّبْحَ مَعَ قِرَاءَةِ ٱلْقُرْآنِ.

ج - اِسْتَيْقَظْتُ مِنَ ٱلنَّوْمِ صَبَاحًا مُبَكِّرًا.

د - وَذَهَبْتُ إِلَى ٱلْمَدْرَسَةِ.

هـ - وَشَرِبْتُ ٱلشَّايَ مَعَ ٱلْخُبْزِ.

ا- إِسْتَيْقَظْتُ مِنَ النَّوْمِ صَبَاحًا مُبَكِّرًا

ب- وَأُنَظِّفُ أَسْنَانِي مَعَ غُسْلِ جِسْمِي

ج- وَصَلَّيْتُ الصُّبْحَ مَعَ قِرَاءَةِ القُرْآنِ

د- وَشَرِبْتُ الشَّايَ مَعَ الخُبْزِ

هـ- وَذَهَبْتُ إِلَى المَدْرَسَةِ.

Kielelezo nambari 10.2 kinaonesha mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyeweza kutoa majibu sahihi kwa kukidhi matakwa ya swali kwani mtahiniwa alipanga vizuri sentensi au ibara alizopewa na kuunda kisa sahihi chenye maana na mtiririko unakubalika katika uandishi wa Insha. Hali hii inaonesha kuwa mtahiniwa anauelewa mzuri juu ya mada ya uandishi wa Insha.

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa jumla wa ufaulu unaonesha kuwa maswali matatu yamejibiwa vizuri, maswali matano yamejibiwa wastani na maswali mawili yamejibiwa vibaya.

Uchambuzi huu unaonesha kuwa ufaulu ili uwe mzuri na wa ufanisi unatokana na jitihada za watahiniwa wenyewe katika kufahamu matakwa ya swali husika, maarifa waliyo nayo juu ya mada husika na kuwa na uelewa mzuri wa lugha ya Kiarabu.

Pia watahiniwa wengi hawakujibu vizuri maswali kutokana na kutokuwa na uelewa mzuri wa matakwa ya maswali, kukosa maarifa juu ya mada zilizojitokeza katika mtihani, kutokuwa na msamiati wa kutosha wa lugha ya Kiarabu, jambo ambalo liliwafanya washindwe kujieleza kwa kutumia lugha hiyo. Pia wapo watahiniwa hawakuwa na umahiri wa kusoma na kuandika lugha ya Kiarabu.

Taarifa hii itasaidia kuinua kiwango cha ufaulu katika somo la Kiarabu na kutoa changamoto kwa walimu na wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada mbalimbali, lengo likiwa ni kukuza lugha ya Kiarabu na kufanya marekebisho ya dosari mbalimbali zilizojitokeza mwaka 2023 na kupelekea kuongeza ufaulu katika mitihani mengine inayofuata.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Kupitia uchambuzi huu mapendekezo yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa ili kuinua kiwango cha ufaulu:-

a) Walimu wazingatie muhtasari wa somo wanapofundisha mada mbalimbali.

b) Wanafunzi wahamasishwe katika kulisoma somo la Kiarabu kwa sababu linaweza kuwapatia fursa nyingi katika maisha yao iwapo watalifaulu vizuri.

c) Walimu watoe mazoezi mengi zaidi kwa wanafunzi ili kuwapa uwezo wa kuyaelewa na kuyajibu maswali ya mtihani kulingana na matakwa ya kila swali.

d) Wakaguzi, maafisa wa mkoa na wilaya, walimu wakuu na wakuu wa seksheni waendelee kuwasimamia walimu wa somo la Kiarabu ili kuhakikisha wanakamilisha muhtasari kwa wakati na wanatimiza kazi zao za ufundishaji ipasavyo.

e) Washauri wazidishe bidii na mkazo zaidi katika kuwapa msaada stahiki walimu ili kuhakikisha kuwa dosari za ufundishaji zinapatiwa ufumbuzi

madhubuti hasa kwa zile mada ambazo ufaulu wake umebainika kuwa ni wa kiwango cha chini.

f) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Zanzibar kupitia Taasisi ya Elimu Zanzibar ihakikishe kuwa inaandaa na kusambaza vitabu vya kiada na ziada kwa wanafunzi wanaosoma somo la lugha ya Kiarabu pamoja na kuwapatia walimu vitabu rejea vinavyoendana na muhtasari wa somo lenyewe.

g) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Zanzibar ifanye jitihada za makusudi katika kuwapatia mafunzo walimu wa somo hili ikiwa ni sambamba na kulishajihisha somo hili sawa na yanavyoshajihishwa masomo mengine ya lugha kama Kiswahili na Kiingereza.

h) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Zanzibar kwa kushirikiana na Baraza la Mitihani la Zanzibar iandae utaratibu wa kuwafunza walimu namna bora za utunzi wa maswali ili walimu hao wawe na uwezo mzuri wa kuwaandaa wanafunzi kuukabili mtihani wa Taifa.

## VIAMBATANISHO
## KIAMBATANISHO NAMBARI 1

### UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI NA MADA MWAKA 2023

| S/N: | MADA | NAMBA YA SWALI | ASILIMIA YA UFAULU | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kanuni za Lugha | **3** | 75.84 | **VIZURI** |
| 2 | Ufahamu | **1** | 70.24 | **VIZURI** |
| 3 | Ufahamu | **2** | 66.93 | **VIZURI** |
| 4 | Kanuni za Lugha | **5** | 48.68 | **WASTANI** |
| 5 | Utungaji | **10** | 38.65 | **WASTANI** |
| 6 | Kanuni za Lugha | **6** | 28.98 | **WASTANI** |
| 7 | Fasihi | **9** | 28.16 | **WASTANI** |
| 8 | Kanuni za Lugha | **7** | 27.38 | **WASTANI** |
| 9 | Kanuni za Lugha | **4** | 8.52 | **VIBAYA** |
| 10 | Fasihi | **8** | 2.86 | **VIBAYA** |

## KIAMBATANISHO NAMBARI 2

### UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI NA MADA MWAKA 2022

| S/N: | MADA | NAMBA YA SWALI | ASILIMIA YA UFAULU | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kanuni za Lugha | **3** | 79.79 | **VIZURI** |
| 2 | Ufahamu | **2** | 46.39 | **WASTANI** |
| 3 | Fasihi | **9** | 40.61 | **WASTANI** |
| 4 | Ufahamu | **1** | 37.20 | **WASTANI** |
| 5 | Kanuni za Lugha | **5** | 26.08 | **WASTANI** |
| 6 | Utungaji | **10** | 12.06 | **VIBAYA** |
| 7 | Kanuni za Lugha | **7** | 10.74 | **VIBAYA** |
| 8 | Kanuni za Lugha | **6** | 7.60 | **VIBAYA** |
| 9 | Kanuni za Lugha | **4** | 3.64 | **VIBAYA** |
| 10 | Fasihi | **8** | 0.40 | **VIBAYA** |